

## Mwachano wa Taratibu za Uundaji wa Istilahi za Kiswahili na Changamoto Zake katika Lugha: Mifano kutoka Istilahi za TATAKI na BAKITA

Joseph Isindikiro

Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere

### Ikisiri

Suala la uundaji wa istilahi katika lugha limekuwa ni la muda mrefu, hivyo, linapaswa kuratibiwa kwa taratibu maalumu na za kudumu. Taratibu hizo zinapaswa kuwa bayana na zisizobadilika jambo linalotajwa kuchochea kudumishwa kwa nidhamu katika mchakato wa uundaji wa istilahi. Utafiti ulilenga kuchunguza mabadiliko katika taratibu mbalimbali za uundaji wa istilahi za lugha ya Kiswahili na changamoto zake katika istilahi zinazoundwa katika mazingira hayo. Taratibu zilihusisha: hatua za uundaji wa istilahi, miongozo inayotumika na ushirikishwaji wa wataalamu wa istilahi kutoka nchi nyingine zinazotumia lugha ya Kiswahili. Data za utafiti zilikusanywa kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, BAKITA na Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine. Mbinu ya usomaji nyaraka maktabani, hojaji na usaili zilitumika kupata data. Data zilikusanywa kwa kuongozwa na nadharia ya Jumla ya Istilahi na kujalizwa na nadharia ya Istilahi za Kisayansi na kuchanganuliwa kwa mkabala wa kitaamuli. Matokeo yamebainishwa kuwa; kila jopo lina hatua zinazofuatwa jambo linaloweza kuchochea kuundwa kwa istilahi zenye changamoto katika lugha. Pia matokeo yamebainishwa kuwa licha ya mwongozo wa BAKITA kuonekana una manufaa zaidi katika kuunda istilahi za Kiswahili, bado pamekuwa na matumizi ya kuchanganya miongozo. Matokeo yameeleza changamoto na mabadiliko yanayokumba msisitizo unaotolewa na mwongozo wa ISO, hivyo, kuufanya ushindwe kutekelezeka kikamilifu. Kuhusu ushirikishwaji wa wataalamu wa lugha ya Kiswahili kutoka nchi nyingine, imebainishwa kuwa ushirikishwaji umekuwa ukifanyika kwa kiwango kidogo na mara nyingine, nchi zinazoshirikishwa hubadilika takribani kila jopo. Matokeo yamehimiza haja ya kuwa na utaratibu maalumu, bayana na pangilifu katika kuunda istilahi za lugha. Pia, matokeo yamehimiza kuwapo kwa juhudi za pamoja za nchi watumiaji wa Kiswahili ili kukipa Kiswahili sura moja katika eneo lote kinamotumika na kuipunguzia lugha mzigo wa istilahi zenye sura ya kanda.

**Misamiati Muhimu:** *Istilahi, Dhana, Taratibu, Hatua, Mwongozo, Mchakato, Jopo*

### Utangulizi

Kumekuwa na miongozo ya uundaji wa istilahi za Kiswahili yenye sura mbili, ya kitaifa na kimataifa. Miongozo ya kimataifa ipo miwili na ina maelekezo tofauti. Mwongozo wa kwanza ni ule wa Shirika la Usanifishaji la Kimataifa (kuanzia sasa mwongozo wa ISO). Mwongozo huo unasisitiza mchakato wa uundaji wa istilahi uzalishe istilahi zenye sura ya kimataifa. Mwongozo wa pili ni ule wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni wa mwaka 2005 (kuanzia sasa mwongozo wa UNESCO). Mwongozo huo unasisitiza kuzingatiwa kwa lugha za kijamii ili kurahisisha uhawilishaji wa dhana kadiri ya uzoefu wa maarifa ya kijamii. Kwa upande wa miongozo ya kitaifa, upo mwongozo wa BAKITA wa mwaka 1982 ambao unasisitiza kwamba mchakato wa uundaji wa istilahi za Kiswahili uzipe kipaumbele lahaja za Kiswahili zikifuatiwa na lugha za Kibantu, lugha za Kiafrika na, hatimaye, lugha za kigeni.

Matumizi ya miongozo hii katika kuunda istilahi za lugha ya Kiswahili yamekuwa hayana mipaka bayana hivyo kuashiria mwelekeo wa kuwapo changamoto katika sura ya istilahi zinazoundwa. Pamoja na miongozo hiyo, miongoni mwa mambo muhimu yanayosisitizwa katika kuunda istilahi za lugha ni suala la izingativu wa nidhamu. Ili kudumisha nidhamu ya istilahi, ni muhimu kuwapo na

kufuatwa kwa utaratibu maalumu katika kuunda istilahi za lugha. Suala la kutokuwapo kwa nidhamu katika uundaji wa istilahi za lugha limekuwa likilalamikiwa na wataalamu mbalimbali (Mdee, 1983; MacWilliam, 1985; Massamba, 1989). Katika mazingira ya miongozo mingi kama hiyo na malalamiko kuhusu kusokekana kwa nidhamu katika uundaji wa istilahi, uwezekano wa waunda istilahi kukanganywa na maelekezo ya miongozo au kuitumia bila mipaka katika utekelezaji wa majukumu yao ni mkubwa. Pamoja na miongozo inayotumika katika uundaji wa istilahi za lugha ya Kiswahili, utafiti ulilenga pia katika kuchunguza taratibu mbalimbali katika mchakato wa uundaji wa istilahi za Kiswahili na namna zinavyozingatiwa na kuonesha namna uzingativu huo unavyoweza kuchangia katika kukubalika au kutokukubalika kwa istilahi zinazoundwa.

### **Kiunzi cha Nadharia**

Utafiti uliofanyika uliongozwa na nadharia ya Jumla ya Istilahi (kuanzia sasa NJI) ya Wuster (1931) na kujalizwa na nadharia ya Istilahi za Kisayansi (kuanzia sasa NIK) iliyoasisiwa na Kiingi (1989). NJI ni kama msingi wa kisayansi wa kuwaongoza waunda istilahi wanapokabiliana na kazi hiyo. Kwa mujibu Were-Mwaro (2002), NJI, inaonesha utekelezaji wa misingi ya kiistilahi na mbinu ambazo kwa kuzizingatia, istilahi bora na zenye ufanisi zitazalishwa katika fani mbalimbali. Kuhusu masuala ya lugha na uundaji wa istilahi, NJI inazo sifa tatu muhimu za kuzingatiwa.

Sifa ya kwanza inasisitiza uundaji wa istilahi kuanza na dhana. NJI inafafanua dhana kama kile kimaanishwacho na istilahi. Katika NJI, uhusiano baina ya kirejelea (istilahi) na kinachorejelewa (dhana) katika lugha, unaelezwa kuwa wa kinasibu. Sifa ya pili inasisitiza kuwa, istilahi za dhana zina manufaa makubwa kwa wanaistilahi kuliko uzingativu wa kanuni za uambishaji na sintaksia. Kwa mujibu wa sifa hii, kanuni za lugha zinapaswa kuzingatiwa zaidi katika matumizi ya mawasiliano ya kawaida si katika matumizi ya mawasiliano ya lugha za kitaalamu. Sifa ya tatu inasisitiza kuwa, mtazamo wa lugha za kiistilahi ni wa kisinkronia. Katika mtazamo wa sifa hii, maana ya sasa ya istilahi ni muhimu na inayopaswa kupewa kipaumbele katika istilahi za lugha.

Kwa mujibu wa nadharia hii, istilahi inayoundwa katika lugha, lazima iakisi kikamilifu dhana yake katika lugha chasili ama kuihusianisha na mifumo mingine ya dhana hiyo. Mtazamo huo, unaonekana kuwa na upungufu iwapo dhana na kirejelewa chake vitachukuliwa kuwa na uhusiano wa kinasibu. Kwa mantiki hiyo, NJI imekuwa na mwelekeo wa kuweka msisitizo katika ukopaji wa dhana na istilahi katika fani zinazoundiwa istilahi na kulitazama eneo la istilahi kama eneo ambalo si huru. Kutokana na mtazamo huo, istilahi ya dhana mpya inapoingizwa katika lugha inafaa kukopwa ili iakisi dhana halisi au uhusiano wa dhana hiyo na dhana nyinginezo katika lugha chasili. Pia, NJI inazuia kufanyika kwa tathimini ya istilahi zilizokwishazoeleka katika lugha hivyo, kukwamisha jitihada za kuboresha istilahi ili ziendane na mahitaji ya fani husika kwa kuwa istilahi hizo tayari zimeshajulikana kimataifa. Kutokana na changamoto za NJI, nadharia hiyo imejalizwa na nadharia ya Istilahi za Kisayansi, kwa kuongeza vigezo ambavyo muunda istilahi yoyote anapaswa kuzingatia ili kupata istilahi zinazokubalika katika lugha.

Licha ya kuwa, NIK imeundwa mahususi kwa ajili ya istilahi za kisayansi ikitilia msisitizo katika kuzingatia kanuni bayana, zisizobadilifu na ushirikishwaji wa makundi mbalimbali katika kuunda istilahi, msisitizo unaowekwa katika NIK, unapaswa kuzingatiwa na waunda istilahi wa fani nyinginezo pia. NIK inatuelekeza katika kuunda istilahi faafu zinazokubalika katika lugha na kukataa istilahi fulani kwa kuwa hazikidhi vigezo muhimu katika lugha (Kiingi, 1989). NIK imeegemezwa katika kushughulikia taratibu muhimu zifuatazo: Utaratibu wa kwanza ni, utaratibu wa uundaji wa dhana. Katika utaratibu huo, mchakato wa uundaji wa istilahi katika lugha uanze na dhana za msingi yaani, dhana, kitamkwa au istilahi. Akifafanua madai haya, Were-Mwaro, (2000) anadokeza kuwa katika NIK, dhana inatazamwa kuwa ya kimataifa wakati ambapo istilahi na kitamkwa hutazamwa kuwa si vya kimataifa. Kwa maana hiyo, dhana mpya zinapoingia katika matumizi ya lugha fulani zinafaa kukopwa, lakini hutakiwa ziundiwe istilahi faafu zaidi. Utaratibu huu ni kinyume na ule uliomo katika NJI ambao pamoja na kuhimiza uzingativu wa dhana, unamlazimisha muunda istilahi kukopa dhana na istilahi yake kutoka lugha chanzi hadi lugha lengwa. Utaratibu wa pili unahusu

sheria ya ubadilishaji dhana ambayo inasisitiza istilahi mpya zinapaswa kujengeka au kuzalishwa pasipo kuzingatia lugha tunayoitumia katika mazungumzo bali lugha ya kitaalamu. Kwa kiasi kikubwa utaratibu huu, unarandana na sifa mojawapo katika NJI inayosisitiza kupuuzwa kanuni za unyambulishaji na sintaksia tunapounda istilahi za lugha. Utaratibu huu umetumika katika utafiti uliofanyika kama mojawapo ya kigezo cha kuzingatia tunapounda istilahi za lugha. Utaratibu wa tatu unahusu sheria ya uunganishaji dhana ambayo inazitazama istilahi kama vitambulisho vya dhana vinavyosisitiza kuziba mapengo ya istilahi katika taaluma au fani husika. Kwa mujibu wa Kiingi (1989), licha ya kuwa vitambulisho vya dhana viko huru katika uundwaji wake, vinapaswa kuwa na dhima ya kuhakikiwa iwapo vinakamilisha mahitaji ya matumizi yake katika lugha husika. Akishadidia hoja hiyo, Were-Mwaro (2000) anaongeza kuwa kwa mujibu wa sheria hii, waunda istilahi wanapaswa kutambua vitambulisho vya dhana zilizomo katika lugha na kuunda istilahi faafu kwa kuzingatia usawa wa sentensi kisarufi.

Kupitia utaratibu huu, vitambulisho vya dhana vinavyoshindwa kukidhi mahitaji ya watumiaji walioundiwa, havina budi kutathiminiwa ili viondolewe au kuboreshwa vikubalike zaidi. Msingi huu umetumika kutokana na umuhimu wa kutathimini ukubalifu wa istilahi zilizoundwa katika lugha ili kuona iwapo ni zana bora kwa mawasiliano ya fani zilizokusudiwa au la. Utaratibu wa nne katika NIK unahusu sheria ya uzingativu wa vigezo vya usahihi, uiktisadi, uzalishaji, umataifa, ustara, utaratibu, ulinganifu, uangavu na uhalisia kama vigezo faafu katika kuunda istilahi za fani mbalimbali. Hivi ni vigezo vya kisayansi ambavyo husaidia kuleta usasa, usawa na upatanisho wa kimataifa katika istilahi zinazoundwa (Kiingi, 1989; Were-Mwaro, 2000). Utaratibu huu haukutumika katika utafiti uliofanyika, kwa kuwa unafaa kutumiwa na waunda istilahi na wataalamu wa lugha katika kuzihakiki istilahi si watumiaji walioundiwa istilahi kupima ukubalifu kwao, bali ukubalifu wa istilahi ulitazamwa kadiri ya maoni ya watoataarifa ambao ni watumiaji wa istilahi hizo. NJI na NIK ziliteuliwa kwa kuwa zinafaa kukamilishana katika utafiti uliofanyika. NJI imetoa misingi inayotumika kama miongozo ya uundaji wa istilahi na NIK ikasaidia kuweka misingi ya uboreshaji wa zoezi la uundaji wa istilahi ambayo, haijifungi katika fani wala lugha mahususi.

### **Methodolojia ya Utafiti**

Utafiti ulifanyika katika mikoa ya Dar es Salaam na Morogoro. Jijini Dar es Salaam, utafiti ulifanyika katika taasisi za BAKITA na Taasisi ya Taaluma za Kiswahili (kuanzia sasa TATAKI). Aidha, baadhi ya data zilikusanywa kutoka ndaki, shule kuu na taasisi mbalimbali za kitaaluma za Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (kuanzia sasa UDSM). Kwa upande mwingine, data za utafiti zilikusanywa kutoka Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (kuanzia sasa SUA). Maeneo hayo yaliteuliwa kwa kuwa ni miongoni mwa taasisi zinazojishughulisha kwa kiasi kikubwa na uundaji wa istilahi za lugha ya Kiswahili nchini Tanzania. Wango la utafiti lilijumuisha wataalamu wanaojihusisha na uundaji wa istilahi za Kiswahili kutoka BAKITA na TATAKI. Dhana ya mtaalamu ilirejelea mtu anayejishughulisha au anayeshiriki kama mwanajopo katika zoezi lolote la uundaji wa istilahi. Wengine ni watendaji kutoka ndaki, shule kuu na taasisi mbalimbali za UDSM ambao ni watumiaji wa istilahi za majina ya vitengo na nyadhifa za viongozi UDSM, watafiti kutoka fani za agronomia na ufugaji na watafiti wa magonjwa ya mimea/wanyama na wadudu waharibifu kutoka SUA kama sehemu ya watumiaji wa istilahi hizo. Utafiti ulitumia mbinu ya usampulishaji sinasibu ambapo mtafiti alitumia njia ya uchaguzi lengwa ili kuwapata watoataarifa saba kutoka idara ya Agronomia na Ufugaji na Idara ya Magonjwa ya Mimea/Wanyama na Wadudu Waharibifu za SUA wanaoshiriki katika tafiti mbalimbali kutoka idara zilizobainishwa kadiri alivyoongozwa na mamlaka zinazosimamia idara hizo.

Mtafiti alilichagua kundi hili akitarajia kwamba mara nyingi wanatumia lugha ya Kiswahili na istilahi zake pindi wanapokutana na watumiaji wa Kiswahili wanaohitaji huduma zao kwa mawasiliano ya kitaalamu. Njia ya uchaguzi lengwa ilitumika pia kuwapata watoataarifa kutoka TATAKI kwa kuwatumia wahadhiri wa Kiswahili walio katika Taasisi hiyo. Mbinu ya usampulishaji tajwa pia ilitumika kwa matarajio ya kuwapata watendaji watatu kutoka katika ndaki, vitengo, shule kuu, taasisi na idara zipatazo ishirini na mbili za UDSM. Katika mbinu hii, mtafiti alikutana na wakuu

wa idara, ndaki, shule kuu na vitengo ambao walimwongoza kupata watoaarifa walioonekana kuwa na taarifa zinazostahili kutoka katika ndaki, vitengo, shule kuu, taasisi au idara zao. Mbinu ya usampulishaji tajwa pia ilitumika kuwapata wataalamu wa uundaji wa istilahi kutoka BAKITA ambapo BAKITA, Baraza lilitua wataalamu wanaohusika na uundaji wa istilahi kuwa sehemu ya watoaarifa zilizohitajika. Mbinu ya usampulishaji kimkakati ilitumika pia katika kuteua istilahi zilizotumika katika utafiti miongoni mwa istilahi nyingi, na za fani mbalimbali zilizoundwa na TATAKI na BAKITA. Mtafiti aliteua istilahi ishirini na tano zilizoundwa kwa ajili ya fani za agronomia na ufugaji, istilahi ishirini na tano za fani ya magonjwa ya mimea/wanyama na wadudu waharibifu zilizoundwa na BAKITA na istilahi thelathini na tisa za majina ya vitengo na nyadhifa za viongozi za UDSM zilizoundwa na TATAKI mwaka 2016. Data za utafiti uliofanyika zilikusanywa maktabani na uwandani. Data za msingi zilikusanywa uwandani kwa kutumia mbinu ya hojaji. Jumla ya watoaarifa arobaini na tisa kutoka katika makundi ya watendaji kutoka UDSM, waunda istilahi kutoka BAKITA na TATAKI na idara mbili za SUA walifikiwa. Mbinu ya usaili ilitumika ili kupata taarifa kutoka kwa wataalamu na watafiti wawili kutoka Idara ya Agronomia na Ufugaji na Idara ya Magonjwa ya Mimea/Wanyama na Wadudu Waharibifu za SUA. Usaili uliofanyika ulikuwa nusu funge kwa kuongozwa na mwongozo wa usaili ulioandaliwa. Mtafiti alikusanya data za upili kwa kusoma makala na ripoti za tafiti mbalimbali zinazohusiana na masuala ya istilahi, uundaji na usanifishaji wake na lugha kwa ujumla. Data hizi zilipatikana katika Makavazi ya TATAKI, Maktaba ya Dr. Wilbert Chagula ya UDSM, na mkondoni.

#### **Matokeo ya Utafiti**

Katika sehemu hii, matokeo ya utafiti yamejadiliwa kadiri ya vipengele mbalimbali vya mwachano wa taratibu vilivyoshughulikiwa. Vipengele hivyo ni: hatua zinazoongoza mchakato ya uundaji wa istilahi za Kiswahili za BAKITA na TATAKI, miongozo inayotumika katika kuunda istilahi za lugha ya Kiswahili, na ushirikishwaji wa wataalamu wa lugha ya Kiswahili kutoka nchi nyingine zinazotumia lugha ya Kiswahili.

#### **Mwachano katika Hatua za Uundaji wa Istilahi katika Mchakato wa Uundaji wa istilahi za BAKITA na TATAKI**

Wataalamu wa lugha wanasisitiza kuhusu uzingativu wa hatua muhimu za uundaji wa istilahi za lugha ya Kiswahili. Hata hivyo, pamekuwa na ukinzani katika hatua zinazopaswa kufuatwa wakati wa kuunda istilahi za lugha (Felber, 1984; Mwansoko, 1989; Sewangi, 2007). Kwa mujibu wa Felber (1984), tunapounda istilahi za lugha, hatua ya kwanza muhimu ni kuichambua dhana ili kubaini uhusiano wake katika lugha lengwa. Hatua ya pili ni kuifafanua dhana hiyo, na, hatua ta tatu ni kuunda istilahi kwa kuzingatia uhusiano wa dhana na istilahi inayoundwa katika lugha lengwa. Mtaalamu mwingine ni Mwansoko (1989) ambaye anasisitiza kuzingatiwa kwa hatua zifuatazo: Kwanza, waunda istilahi hukusanya istilahi kutokana na dhana zilizobainishwa katika lugha chasili. Pili, kuandaa maelezo ya istilahi ambapo waunda istilahi hubuni maneno au ufafanuzi wa dhana ya kila istilahi. Tatu, ni kuandaa mifano ambayo itatumika kama vielelezo katika ufafanuzi, na nne ni mapendekezo ya istilahi ambapo waunda istilahi huwa na jukumu la kupendekeza maneno yanayofaa kutafsiri dhana husika kutoka lugha chasili. Utaratibu mwingine ni mapendekezo ya yanayotolewa na Sewangi (2007) yakipendekeza kuzingatiwa kwa hatua zifuatazo: kwanza, kukusanya istilahi zinazopaswa kuundiwa istilahi kutoka lugha chanzi. Pili, kufafanua dhana zinazobeba istilahi hizo, na tatu, kuunda visawe katika lugha lengwa. Katika utafiti uliofanyika, jumla ya watoaarifa wanne kutoka TATAKI na wanne kutoka BAKITA walionesha hatua zinazofuatwa na taasisi zao katika majopo mbalimbali ya uundaji wa istilahi za Kiswahili waliyoshiriki hizo Kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 1.

**Jedwali Na 1: Hatua Zinazofuatwa katika Majopo Mbalimbali ya Uundaji wa Istilahi za Kiswahili za BAKITA na TATAKI**

Taasisi	Hatua za Uundaji wa Istilahi Zilizobainishwa wa Watoataarifa			
	MTOATAARIFA-I	MTOATAARIFA-II	MTOATAARIFA-III	MTOATAARIFA-IV
BAKITA	i. Kupendekez a neno. ii. Kulipeleleza kama lipo katika lugha nyingine za Kibantu. iii. Kuwapa wataalamu wengine na wadau kulitathimini. iv. Kuhusisha jopo la kusanifu. v. Kulinadi katika jamii.	i. Kuangalia maana au kazi ya neno husika. ii. Kuangalia kisawe cha istilahi hiyo katika lugha lengwa. iii. Urahisishaji wa istilahi kifonolojia ili iendane na lugha lengwa. iv. Uundaji wa istilahi kimofolojia ili uendane na lugha lengwa.	i. Kukusanya istilahi zinazohitaji kusanifiwa. ii. Kuitisha majopo ya ndani kwa ajili ya usanifishaji. iii. Kupitia istilahi na kuzithibitish. iv. Kuitisha majopo ya usanifishaji.	i. Hapana utaratibu maalumu isipokuwa mahitaji na haraka iliyopo.
TATAKI	i. Inategemea istilahi husika na mahitaji ya mradi.	ii. Utafiti wa maktabani. iii. Kupata mahitaji. iv. Kuuliza watumiaji. v. Kuangalia katika lugha na lahaja mbalimbali.	i. Kuangalia mwongozo unasemaje. ii. Kuangalia upatikanaji wa istilahi. iii. Kuchagua istilahi kutoka vyanzo husika. iv. Kuitathimini istilahi katika majopo. v. Kuipitisha istilahi kwa matumizi.	i. Kubuni istilahi. ii. Kujadili ufaafu wa istilahi iliyobuniwa. iii. Kuipitisha istilahi.

**Chanzo:** Data za Uwandani (2022)

Kutokana na Jedwali Na. 1 hapo juu, tunaweza kusema kuwa mchakato wa uundaji wa istilahi za Kiswahili unaofanywa na BAKITA na TATAKI kwa kiasi kikubwa haufuati hatua maalumu na zinazofanana. Mchakato unaendeshwa kwa hatua zinazobadilika kila mara kulingana na sababu mbalimbali. Matokeo ya utafiti yalibainisha kuwa, hata katika chombo kimoja kumekuwa na mabadiliko ya hatua zinazofuatwa katika kila jopo la uundaji wa istilahi zinazohitajika. Mabadiliko hayo hufanya baadhi ya waunda istilahi kuanzia na utafutaji wa kisawe katika lugha lengwa bila

kufafanua dhana hiyo, na majopo mengine kujikita zaidi katika kuichunguza na kuifafanua dhana kabla ya kuiundia istilahi. Katika mabadiliko kama haya, upo uwezekano mkubwa wa kuundwa kwa istilahi zinazotofautiana kurejelea dhana moja au kuwa na istitahi zenye changamoto katika kukubalika kwake.

#### **Mabadiliko katika Uzingativu wa Miongozo ya Uundaji wa Istilahi za Lugha ya Kiswahili**

Dhana ya mwongozo inarejelea maelekezo au mpango unaotoa maelekezo juu ya utekelezaji wa shughuli maalumu (BAKIZA, 2010). Mpango huo unaweza kutolewa kwa mdomo au maandishi ukiwahimiza na kuwaelekeza watu fulani kutekeleza jukumu kwa namna fulani (TUKI, 2013). Kwa fasili hiyo, mwongozo ni nyenzo muhimu inayowezesha upatikanaji wa matokeo yanayokubalika katika jambo au shughuli iliyopangwa kufanyika ikiwa kwa muda mfupi au mrefu kwa kuwa, mwongozo unatoa dira ya namna sahihi na yenye ufanisi kiutendaji.

Katika kuratibu mchakato wa uundaji wa istilahi, pamekuwa na miongozo ya namna mbalimbali. Kundi la kwanza linajumuisha miongozo iliyowekwa na vyombo vya kimataifa ambayo ni mwongozo wa ISO na Mwongozo wa UNESCO. Mwongozo wa ISO unasisitiza istilahi za lugha kuwa na sura ya kimataifa kwa kuhifadhi sehemu ya mzizi wa istilahi inayoundwa katika lugha mojawapo kati ya Kilatini na Kirumi, hivyo kukinzana na mwongozo wa UNESCO unaohimiza uzingativu wa lugha za kijamii katika kuunda istilahi za lugha. Kundi la pili linajumuisha miongozo yenye sura ya kitaifa, ikiwamo mwongozo wa BAKITA wa mwaka 1982 unaosisitiza kipaumbele kuwekwa katika lugha ya Kiswahili na lahaja zake, kisha lugha za Kibantu, lugha nyinginezo za Kiafrika na mwisho kabisa kuunda istilahi kwa kutumia lugha za kigeni (Tumbo-Masabo na Mwansoko, 1992; Akida, 2008). Kuwapo kwa tofauti katika msisitizo unaowekwa katika miongozo hiyo na namna inavyotumika bila mipaka katika kuunda istilahi za lugha ya Kiswahili kulitazamwa katika sehemu hii na kubaini yafuatayo:

Matokeo ya utafiti yamebani kuwa msisitizo unaotolewa na ISO uliwekwa wakati ambapo sehemu kubwa ya maarifa ya ulimwengu yalihifadhiwa katika maandishi kupitia Kilatini na Kirumi. Kutokana na sababu hiyo, uundaji wa istilahi hususani za kisayansi ungesaidia kufanikisha mawasiliano kirahisi miongoni mwa wanasayansi wote ulimwenguni. Ili kufanikisha mahitaji ya mwongozo huu, matokeo ya utafiti uliofanyika yalibainisha matumizi makubwa ya mbinu ya utohozi mkamilifu au utohozi nusu ili kupata istilahi zitakazokidhi matakwa yake. Mfano Na. 1 unaonesha baadhi ya istilahi zilizoundwa kwa kuzingatia msisitizo wa mwongozo wa ISO.

<b>Dhana</b>	<b>Istilahi Iliyoundwa</b>
<i>Xenia</i>	Zenia
<i>Acid</i>	Asidi
<i>Filaments</i>	Filamenti
<i>Capillary</i>	Kapilari
<i>Tetraploid</i>	Tetraploidi
<i>Electronegative</i>	Elektrohali
<i>Sheet metal</i>	Bamba metali
<i>Bacteria blight</i>	Baka bacteria
<i>Exchangeable Ion</i>	Ayoni badilifu
<i>Recessive gene</i>	Jeni hafifu

**Chanzo:** BAKITA (2005)

Licha ya istilahi zilizo katika mfano Na.1 kutumika katika lugha ya Kiswahili, watoataarifa waliofikiwa walibainisha kuwa istilahi za namna hii hazisaidia lugha kukua na kujitegemea. Kutokana na maoni yao, jitihada za kuhifadhi umataifa katika istilahi zinazoundwa ni kama harakati za makusudi za kusisitiza ukoloni mamboleo dhidi ya lugha nyingine na kuzifanya lugha changa zisijitegemea na kuwa na sura isiyo na uasilia wa lugha zake (taz. pia, Marcel, 1983; Kalondero, 1983, Mwansoko, 2007).

Pamoja na hilo, matokeo ya utafiti yalibainisha kuhusu mwelekeo wa mabadiliko katika lugha ambazo awali zilitajwa kuwa lugha za kuzingatiwa katika kuhifadhi umataifa katika mwongozo wa ISO. Katika siku za hivi karibuni, lugha kama Kiingereza, Kifaransa na Kichina zimekuwa na mwelekeo wa kuwa lugha za kimataifa kuliko Kilatini na Kirumi. Kutokana na mabadiliko ya mwelekeo huo, istilahi nyingi za Kiswahili zimeundwa kwa kuhifadhi sehemu ya mizizi yake katika lugha ya Kiingereza. Miongoni mwa sababu za kupendekeza matumizi ya lugha ya Kiingereza ni kama vile: Mosi, vitabu vingi vya kaida na ziada vya elimu vimeandikwa kwa Kiingereza. Pili, hadi sasa Kiingereza ndiyo lugha ya kufundishia elimu ya juu. Tatu, idadi kubwa ya watumiaji lengwa wa istilahi za Kiswahili walisomeshwa au wanaendelea kusomeshwa kwa Kiingereza, hivyo wanapendelea istilahi za Kiingereza na huzimudu zaidi. Nne, Kiingereza ni kinachukuliwa kuwa lugha ya kimataifa ya kisasa zaidi, hivyo istilahi za Kiswahili zinazotoka katika Kiingereza zinakuwa na umataifa zaidi (Mwansoko, 2007).

Matokeo ya utafiti yamebainisha kuhusu kuwapo kwa mabadiliko katika uzingativu wa lugha itakayotumika kuhifadhi umataifa katika istilahi zinazoundwa katika lugha ya Kiswahili. Kutokana na mabadiliko hayo, Mfano Na.2 unaonesha orodha ya istilahi za Kiswahili zinavyopaswa kuwa kwa kuzingatia mwongozo wa ISO unaosisitiza uzingativu wa Kilatini na Kirumi na namna zinavyotumika sasa.

<b>Kiswahili</b>	<b>Kilatini/Kigiriki</b>	<b>Kiingereza</b>
Fizikia	Physicos	Physics
Molekuli	Moles	Molecules
Elektroni	Electroni	Electron
Kemia	Khemia	Chemistry

**Chanzo:** Kiputiputi (2007:115-116)

Mfano Na. 2 unaonesha istilahi zinazotumika katika lugha ya Kiswahili zimehifadhi umataifa kwa kutohoa dhana kutoka Kiingereza na si Kilatini na Kigiriki kama mapendekezo yalivyo. Mabadiliko kama haya katika mchakato wa uundaji wa istilahi za Kiswahili, yanaweza kuchangia kuzalishwa kwa istilahi zenye changamoto katika kukubalika kwake. Licha ya kuwa istilahi zilizoundwa kutokana na Kilatini na kigiriki ndizo zinazopaswa kukubalika zaidi, lakini istilahi za Kiingereza ndizo zinaonekana kutumika zaidi katika Kiswahili kinyume na msisitizo wa mwongozo wa ISO. Sambamba na mabadiliko hayo, matokeo ya utafiti yameonesha kuwa, lugha ya Kiswahili inakuwa na kuongeza watumiaji waliosoma na kupata elimu zao kwa lugha tofauti na Kiingereza, mathalani, watumiaji wa Kiswahili kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Rwanda na Sudan Kusini. Sababu za kuendelea kuhifadhi umataifa kwa kutumia Kiingereza, zinapaswa kuhakikiwa upya kwa kuwa zitakuwa zinawabagua watumiaji wa Kiswahili wasiokuwa na usuli katika lugha ya Kiingereza. Watumiaji kutoka nchi hizo, wamekuwa na hulka ya kutumia istilahi zenye mwangi wa lugha za watawala wao hususani Wafaransa (Kitumbo, 1973; Kalondero, 1983; Marcel, 1983 ).

Kwa upande mwingine, mwongozo wa BAKITA wa mwaka 1982 ulikusudiwa kushughulikia istilahi za Kiswahili kwa kuzingatia uhusiano mkubwa uliopo baina ya lugha ya Kiswahili na lugha nyingine za Kibantu (Massamba, 2017). Matumizi ya mwongozo wa BAKITA yalikusudiwa kuzalisha istilahi zitakazohifadhi uasilia wa lugha na ambazo zingepeny kirasahi katika matumizi. Kutokana na mwongozo huo, istilahi zilipaswa kuundwa kutoka lugha ya Kiswahili kwa kutumia mbinu mbalimbali kama vile ukopaji kutoka lahaja za Kiswahili, lugha za Kibantu na lugha nyingine za Kiafrika kama Mfano Na. 3 unavyoonesha;

<b>Dhana</b>	<b>Istilahi ya Kiswahili</b>	<b>Chanzo</b>
<i>Drill</i>	Kidubingo	Kigogo
<i>Planter</i>	Kitemela	Kisukuma
<i>Non-Tillage system</i>	Ukatuzi msanilo	Kijita
<i>Smuts</i>	Fugwe	Kisumbwa
<i>Leaf miner</i>	Kidomozi	Kibondei
<i>Stake</i>	Mshiika	Kichaga
<i>Mass selection</i>	Ushilaji	Kimasai/Kiarusha

**Chanzo:** BAKITA (2005)

Mbinu nyingine zinazoweza kutumika katika kuunda istilahi za Kiswahili zinazokidhi mahitaji ya mwongozo wa BAKITA ni pamoja na miambatano ya maneno, ufupishaji au uradidi. Mfano Na. 4 unaonesha baadhi ya mapendekezo ya istilahi za Kiswahili kadiri ya ili kukidhi matakwa ya mwongozo wa BAKITA.

Istilahi ya Kigeni	Mapendekezo ya Istilahi za Kiswahili		
<i>Psychology</i>	Elinafsi	Elimunafsi	Elimu ya Nafsi
<i>Botany</i>	Elimimea	Elimumimea	Elimu ya Mimea
<i>Architecture</i>	Elimujenzi	Elimuujenzi	Elimu ya Ujenzi
<i>Arc</i>	Seduara	Sehemuduara	Sehemu ya Duara

**Chanzo:** Gibbe (2008)

Katika matokeo ya utafiti uliofanyika, jumla ya watoataarifa wanane kutoka BAKITA na TATAKI walibainisha miongozo wanayoizingatia katika kuunda istilahi za Kiswahili kama Jedwali Na. 2 linavyoonesha:

**Jedwali Na 2: Kiwango cha Uzingativu wa Miongozo ya Uundaji wa Istilahi**

Taasisi	WATOA TAARIFA WALIOFIKIWA	Miongozo Inayotumika Katika Kuunda Istilahi za Kiswahili				
		ISO	UNESCO	BAKITA	Mchanganyiko	Miongozo Mseto
BAKITA	4	-	-	1	3	-
TATAKI	4	-	-	2	2	-
JUMLA	8	-	-	3	5	-

**Chanzo:** Data za Uwandani (2022)

Kutokana na Jedwali Na. 2, matokeo ya utafiti yalibainisha kuwa, katika mchakato wa uundaji wa istilahi za Kiswahili ya BAKITA, miongozo yote inatumika kwa kuingiliana kwa kiwango kikubwa na baadhi ya majopo yanayoratibiwa na baraza hilo, yamekuwa na umahususi kwa kutumia miongozo iliyowekwa na BAKITA. Kwa upande wa TATAKI, matokeo ya utafiti yalionesha kuwa, kiwango cha uzingativu wa miongozo ya BAKITA katika kuunda istilahi za Kiswahili ni asilimia hamsini na kiwango kama hicho kinatumika pia kwa miongozo mseto. Matokeo ya kutumika kwa pamoja kwa miongozo hiyo ni pamoja na kuzalishwa kwa istilahi zinazoweza kutiliwa shaka katika kukubalika kwake kwa watumiaji.

Mwachano katika uzingativu wa miongozo inayotumika katika uundaji wa istilahi za lugha ya Kiswahili, unaweza kusababisha mambo yafuatayo: Mosi, lugha ya Kiswahili kusheheni istilahi zenye sura ya lugha za kigeni hasa istilahi zinazoundwa kwa kuzingatia mbinu za tafsiri na utohoaji. Istilahi hizo zinatokana na wepesi wa kutumia mbinu hizo na kisingizio cha kuhifadhi umataifa. Pili, istilahi nyingi zinazozalishwa kwa kuzingatia msisitizo wa mwongozo wa ISO, zinaelekea kutogusa kikamilifu hisia za walioundiwa istilahi hivyo kutokukubalika kirahisi (Kiingi, 1989; Hamad, 2008; Msigwa, 2016). Licha ya msisitizo katika kutumia mwongozo wa BAKITA, waunda istilahi hutazama msisitizo wa kundi kama ziada hasa katika kujazia istilahi chache tu. Matokeo ya utafiti yameonesha pia kuwa, licha ya istilahi nyingi kuundwa kutokana na lugha ya Kiswahili na lahaja zake, kundi la lahaja za Kiswahili lina mchango mdogo katika kuunda istilahi ulikinganisha na idadi ya lahaja zilizopo. Matokeo ya utafiti yamedokeza kuwa hata hizo lahaja chache zinazotazamwa huwa ni zilizoko katika visiwa vya Unguja na Pemba pekee bila kuzingatia kuwa lahaja za Kiswahili zimezagaa karibu eneo lote la Pwani ya Somalia hadi eneo la Pwani kusini mwa upwa wa Tanzania (Massamba, 2017).



**Ushirikishwaji wa Wataalamu ya Kiswahili kutoka mataifa mbalimbali ya watumiaji wa Kiswahili** Wataalamu wa lugha katika kujadili kuhusu taratibu wa uundaji wa istilahi za lugha, wanaonesha umuhimu wa ushirikiano baina ya wataalamu wa uundaji wa istilahi kutoka mataifa mbalimbali ya watumiaji wa lugha ya Kiswahili. Katika miaka ya karibuni, matumizi ya Kiswahili sanifu yameenea mahali pengi duniani kiasi cha kuvuka mipaka ya kutumika kutolea elimu na kurahisisha mawasiliano kama ilivyokusudiwa wakati wa uundwaji wa Kamati ya lugha (Kiswahili) ya Afrika Mashariki. Leo hii, Kiswahili ni lugha ya taifa katika nchi za Tanzania, Kenya, Uganda na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Kiswahili kinatumika kwa mawasiliano muhimu katika nchi kama, Zambia, Rwanda na Burundi. Kiswahili kinatumika katika vyombo vya habari vya kimataifa kama vile: Shirika la Utangazaji la Uingereza, na Sauti ya Amerika. Kiswahili kinafundishwa katika vyuo vikuu mbalimbali ulimwenguni na kuwa mojawapo ya lugha rasmi za Umoja wa Afrika na mashirika ya mbalimbali ya kimataifa (Kamwendo, 2001; Masanjila na wenzie, 2011). Kwa mujibu wa Kiango (2002), Kiswahili sanifu kinachukuliwa kuwa lugha ya kuziunganisha nchi zote za Afrika Mashariki na Kati kwa kuwa kimeenea karibu eneo hilo lote japo kwa viwango tofauti. Kupanuka kwa mipaka ya matumizi ya lugha ya Kiswahili kunachochea haja ya ushirikiano baina ya wataalamu kutoka nchi za watumiaji wa Kiswahili katika kuunda istilahi za fani mbalimbali katika lugha ya Kiswahili ili kukipa Kiswahili sura inayofanana miongoni mwa watumiaji wake wote.

Wataalamu mbalimbali wanadokeza mambo yafuatayo katika ushirikishwaji tunapounda istilahi za lugha ya Kiswahili. Kwanza, hapana budi kuwa na juhudi za pamoja katika kutafuta, kuunda na kusanifisha istilahi za lugha zitakiwazo katika fani mbalimbali. Pili, juhudi za pamoja katika kutafuta, kuunda na kusanifisha istilahi za lugha zinaiwezesha lugha kutatua changamoto ya upungufu wa istilahi kwa watumiaji wake wote na kuepusha uwezekano wa kuwapo kwa istilahi za kikanda au kitaifa miongoni mwa watumiaji wa lugha moja. Tatu, suala la uundaji wa istilahi linapaswa kufanyika kwa kuunganisha juhudi za wataalamu kutoka mashirika ya mataifa mbalimbali yanayotumia lugha ya Kiswahili siyo mzigo huo kuachwa kwa mtu au nchi moja pekee. Nne, licha ya licha ya Tanzania kuwa kitovu cha lugha ya Kiswahili ulimwenguni, michango kutoka kwa wataalamu wa lugha hiyo wa nchi nyingine za Afrika Mashariki na wa ughaibuni katika kukuza na kuendeleza lugha ni jambo muhimu na lisiloepukika (Mbaabu, 1991; Hans, 2014; Akida, 2008).

Zipo changamoto zinazoweza kuzikumba istilahi za lugha kutokana na kutowashirikisha kikamilifu wataalamu wa lugha kutoka nchi nyingine. Baadhi ya changamoto hizo ni: kuunda istilahi zisizokubalika au zitakazopata changamoto katika matumizi nje ya eneo fulani inamotumika lugha moja, uwezekano wa dhana moja kuelezwa kwa namna tofauti katika eneo inamotumika lugha hiyo (Msigwa, 2016). Jedwali Na. 3 linaonesha kiwango cha ushirikishwaji wa wataalamu wa lugha kutoka nchi mbalimbali za watumiaji wa Kiswahili katika majopo ya uundaji wa Kiswahili ya TATAKI na BAKITA.

**Jedwali Na 3: Kiwango cha Ushirikishwaji wa Wataalamu Kutoka Nchi Nyingine za Watumiaji wa Kiswahili**

Taasisi	Nchi Zinazoshiriki Katika Majopo ya Uundaji wa Istilahi za Kiswahili za BAKITA na TATAKI													
	KENYA		UGANDA		KONGO		RWANDA		BURUNDI		ZANZIBAR		NJE YA AFRIKA	
	ID	%	ID	%	ID	%	ID	%	ID	%	ID	%	ID	%
BAKITA	1	25	-	0	-	0	-	0	-	0	3	75	-	0
TATAKI	2	50	1	25	-	0	1	25	-	0	-	-	-	0

**Chanzo:** Data ya Uwandani (2022)

Matokeo ya utafiti yalibainisha kuwa katika utaratibu wa kuunda istilahi unaofanywa na BAKITA na TATAKI, ushirikishwaji wa wataalamu wa lugha ya Kiswahili kutoka nchi nyingine za watumiaji wa Kiswahili unafanyika kwa viwango tofauti au wakati mwingine haufanyiki kabisa. Watoataarifa watatu sawa na asilimia sabini na tano ya watoa taarifa kutoka BAKITA walionesha kuwa, majopo ya uundaji wa istilahi za fani mbalimbali za Kiswahili katika taasisi hiyo yanashirikisha wataalamu kutoka Zanzibar. Mtoa taarifa mmoja sawa na asilimia ishirini na tano alionesha kuwa baaadhi ya majopo ya uundaji wa istilahi aliyoshiriki, yalishirikisha wataalamu kutoka Kenya. Hata hivyo, mtoataarifa mmoja kutoka BAKITA sawa na asilimia ishirini na tano ya watoataarifa alibainisha kuwa, wakati mwingine majopo hayo hayashirikishi wataalamu kutoka nchi yoyote isipokuwa wataalamu kutoka taasisi nyingine zinazojihusisha na uundaji wa istilahi za lugha ya Kiswahili zinazoendesha shughuli zake nchini Tanzania. Kwa mujibu wa mtoataarifa huyo sababu ya hali hii ni ukosefu wa fedha za kuwagharimia wataalamu wa lugha kutoka katika nchi zote zinazotumia Kiswahili. Matokeo ya utafiti yalionesha kuwa nchi nyinginezo kama Uganda, na Kongo licha ya kutumia Kiswahili kama mojawapo ya lugha muhimu kwa mawasiliano ya kitaifa, Burundi na Rwanda ambazo pia hutumia Kiswahili kama lugha muhimu katika mawasiliano, na nchi nyinginezo ambako Kiswahili kinafundishwa na kutumika katika vyombo vya habari, wataalamu wa lugha kutoka nchi hizo hawashirikishwi kabisa katika majopo ya uundaji wa istilahi yanayoratibiwa na BAKITA.

Kwa upande wa TATAKI, watoataarifa wanne walishiriki katika kutoa taarifa kuhusu ushirikishwaji wa wataalamu na watumiaji wa lugha ya Kiswahili kutoka mataifa ya watumiaji wa Kiswahili. Matokeo ya utafiti yalibaini kuwa asilimia hamsini ya ushirikishwaji katika majopo ya uundaji wa istilahi za TATAKI ulifanyika kwa kuwaalika wataalamu kutoka Kenya na asilimia ishirini na tano kutoka katika nchi za Uganda na Rwanda. Takwimu hizi zinashabihiana na takwimu za BAKITA katika kuwashirikisha wataalamu wa lugha kutoka katika nchi za Kongo, Burundi na nchi nyinginezo ambao hawashirikishwi kabisa katika majopo ya uundaji wa istilahi za lugha ya Kiswahili licha ya kuwa, Kiswahili kinafundishwa na kutumika katika vyombo vya habari vya nchi hizo.

Mabadiliko katika kuwashirikisha wataalamu wa lugha au kutozingatia umuhimu wa kuwashirikisha wataalamu kutoka sehemu nyingine, yanaweza kuchangia kutokukubalika kwa istilahi za lugha au kuifanya lugha iwe na mzigo wa istilahi zinazoegemea katika sura ya kitaifa na kikanda. Changamoto hii inaweza kuthibitika kupitia mifano ya istilahi zinazorejelea dhana za kiutafiti na

namna zilivyokuwa tofauti kabla ya kupatiwa ufumbuzi kwa kuundwa Istilahi za Utafiti na Maneno Husiani za TATAKI mwaka 2020. Mifano katika Jedwali Na. 4 inaonesha mojawapo ya dhana za utafiti na istilahi tofauti zilizotumika kurejelea dhana hiyo kama zilivyoundwa na vyuo vikuo mbalimbali.

**Jedwali Na 4: Mifano ya Istilahi za Kiswahili Zilizoundwa Pasipo Ushirikiano wa Waunda Istilahi wa Mataifa/Asasi Mbalimbali**

Dhana	Chuo	Istilahi Iliyoundwa
Statement of The Problem	UDSM	Tamko la Utafiti Tatizo la Utafiti Tamko la Tatizo la Utafiti
	UDOM	Tamko la Tatizo la Utafiti
	Chuo Kikuu cha Kenyatta	Suala la Utafiti
	Chuo Kikuu cha Egerton	Somo la Utafiti

**Chanzo:** Msigwa (2016)

Jambo la pili lililobainika katika ushirikishwaji ni mabadiliko katika mataifa yanayoshirikishwa katika majopo mbalimbali ya uundaji wa istilahi za lugha kila wakati. Matokeo ya utafiti yalibainisha kuwapo kwa mabadiliko hayo na kuonesha kuwa, hali hii inaweza kusababisha kukosekana kwa mwendelezo mmoja katika jitihada za kukuza lugha ya Kiswahili. Kutokana na maoni yaliyotolewa na watoataarifa kupitia mbinu ya hojaji, nchi zote watumiaji wa lugha ya Kiswahili zinapaswa kushiriki kikamilifu katika majopo yote ili kuwa na mwendelezo sawa na kuzalisha istilahi zenye sura moja katika eneo lote la watumiaji wa lugha ya Kiswahili. Kukosekana kwa ushirikiano wa kutosha na mabadiliko ya mara wa mara katika makundi yanayoshirikishwa katika uundaji wa istilahi za lugha ya Kiswahili, licha ya kuwa na uwezekano wa kuzalisha istilahi zenye sura ya kikanda, zinaweza kuzalisha istilahi zenye changamoto katika kukubalika kwake kwa kuwa istilahi hizo hazikuhusisha maoni ya watumiaji kutoka mataifa mengine.

**Hitimisho na Mapendekezo**

Suala la uundaji wa istilahi katika lugha linapaswa kuzingatia nidhamu kwa kuwekwa na kusisitiza taratibu maalumu, pangilifu na bayana. Kuwapo kwa taratibu hizo hususani katika hatua za kufuatwa katika michakao ya kupata istilahi, miongozo inayopaswa kufuatwa na ushirikishwaji wa makundi mengine ya watumiaji wa Kiswahili, zitaivezesha lugha ya Kiswahili kuwa na istilahi zinazokubalika katika maeneo yote lugha inamotumika. Kuhusu hatua za uundaji wa istilahi za lugha ya Kiswahili na ukinzani uliopo, matokeo ya utafiti yamependekeza kufanywa kwa uboreshaji katika hatua zinazopendekezwa na Mwansoko (1989) na Sewangi (2007) ili kuzifanya hatua hizo kuipa dhana kipaumbele, kuwashirikisha wataalamu wa uundaji wa istilahi na wataalamu wa fani zinazoundiwa istilahi. Matokeo ya utafiti yamependekeza kufuatwa kwa hatua zifuatazo: Kwanza, kukusanya dhana kutoka lugha chasili. Pili, kufafanua dhana mpya katika majopo ya lugha lengwa. Tatu, kupendekeza istilahi za dhana hizo katika lugha lengwa. Nne, kujadili istilahi zilizoundwa katika majopo mbalimbali. Tano, kuidhinisha istilahi kupitia vyombo vyenye dhamana ya kurasimisha istilahi. Sita, kufanyika kwa tathimini ya istilahi zilizoundwa kupitia majopo ya istilahi. Aidha matokeo ya utafiti yameonesha kuhusu mwachano mkubwa katika matumizi ya miongozo ya uundaji wa istilahi za lugha ya Kiswahili. Matokeo ya utafiti yanapendekeza uzingativu mkubwa wa msisitizo unaowekwa katika mwongozo wa uundaji wa istilahi wa BAKITA. Mapendekezo hayo yanatokana na changamoto za kutumia mbinu za utohozu katika kuunda istilahi za Kiswahili, changamoto katika uzingativu wa lugha chasili inayopaswa kuhifadhi umataifa wa istilahi za kigeni na uhusiano uliopo baina ya lugha ya Kiswahili na lugha nyingine za Kibantu na Kiafrika. Kuhusu suala la ushirikishwaji wa wataalamu wa lugha kutoka nchi mbalimbali za watumiaji wa Kiswahili, matokeo ya utafiti yamependekeza kuwa Kiswahili kama lugha inayoendelea kukua kwa kasi, jitihada za kuhakikisha kunakuwa na

istilahi zinazokidhi mahitaji ya nyanja mbalimbali zinapaswa kuratibiwa na chombo kimoja katika nchi zote lugha inamotumika. Chombo hiki kinaweza kushughulikia ustawi wa lugha kwa kushirikiana na mabaraza au asasi zilizoteuliwa kutoka kila nchi.

### Marejeleo

- Akida, H. (2008) "Ukuzaji na Uendelezaji wa Msamiati wa Kiswahili". Katika Kiango, J.G. (Mh.) *Ukuzaji wa Istilahi za Kiswahili*. Dar es Salaam: TUKI. Uk. 52-78.
- BAKITA (2005) *Istilahi za Kiswahili*. Dar es Salaam: BAKITA.
- BAKIZA (2010) *Kamusi la Kiswahili Fasaha*. Nairobi: Oxford University Press.
- Felber, H. (1984) *Terminology of Manual*, UNESCO and Infoterm Paris. INFOREM Series 21/Umsist.
- Gibbe, A. (2008) "Maendeleo ya Istilahi za Kiswahili". Katika J.G. Kiango (Mh.) *Ukuzaji wa Istilahi za Kiswahili*. Dar es Salaam: TUKI. Uk. 79-99.
- Hamad, A. (2008) "Ukubalifu wa Msamiati na Istilahi katika Tanzania Visiwani". Katika J.G Kiango (Mh.) *Ukuzaji wa Istilahi za Kiswahili*. Dar es Salaam: TUKI. Uk. 128-136.
- Hans, M.M. (2014) Mchango wa Lahaja katika Kukuza na Kuendeleza Kiswahili Sanifu, hazina Fiche iliyomo katika Lahaja za Kiswahili za Zanzibar. Tasnifu ya Uzamivu (*Hajjchapishwa*). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Dar es Salaam.
- Kalondero, K. (1983) "Sura ya Kiswahili Katika Zaire". *Makala za Mkutano wa Kimataifa wa Usanifishaji wa Waandishi wa Kiswahili I*. Dar es Salaam: TUKI.
- Kamwendo, H. G. (2001) "Rething the Status of Kiswahili in Malawi". Katika *Makala ya Kongamano la Kimataifa Kiswahili 2000*. Dar es Salam: TUKI. Uk. 103-108.
- Kiango, J. G. (2002) "Nafasi ya Kiswahili katika Ujenzi wa Jamii Mpya ya Afrika Mashariki". *Swahili Forum IX*. AAP72. Uk. 143-154.
- Kiingi, B. (1989) Systematic Approach to The Problems of the Expression Modernization in The Formal and Natural Science. The Case of Luganda. Tasnifu ya Uzamivu (*Hajjchapishwa*). Chuo Kikuu cha Bielefeld.
- Kiputiputi, O.M. (2007) "Kwa nini Kiswahili kinafaa kuwa Lugha ya Kufundishia Masomo ya Sayansi na Teknolojia". Katika Tumbo-Masabo na Chiduo (Wah.) *Kiswahili katika Elimu*, Dar es Salaam: TUKI. Uk. 107-128.
- Kitumbo, H. L. (1973) "Lugha ya Kiswahili Katika Zaire". *Kiswahili: Jarida la Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili*: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam: Juz. 43(2): Uk 64-66.
- Marcel, B. (1983) "Lugha ya Kiswahili Nchini Burundi". *Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili I*. Dar es Salaam: TUKI.
- Massamba, D.P.B. (1989) "An Assessment of the Development and Modernization of The Kiswahili Language in Tanzania". Katika Coulman (Mh.) *Language Adoption*: Cambrige. Uk. 60-78.
- Massamba, D.P.B. (2017) *Historia ya Kiswahili: Mtaazamo Mpya 100KK badi 2000BK*. Dar es Salaam: Kiswahili Development Limited
- Mbaabu, I. (1991) "Ukubalifu wa Msamiati Kutoka Kenya". *Usanifishaji wa Istilahi za Kiswahili: Makala za Semina ya Kiswahili*. Dar es Salaam: TUKI.
- Msanjila, Y.P, Kihore, Y.M na Massamba, D.P.B. (2011) *Isimujamii: Sekondari na Vyuo Toleo la Pili*. Dar es Salaam: TUKI.
- Msigwa, A.B.G. (2016) "Changamoto za Istilahi katika Uandishi wa Tasnifu za Uzamili wa Tanzania". *Kiswahili: Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*. Dar es Salaam:TATAKI. Juz. 79.
- Mwansoko, H.M. (1989) "The Principles, Methods and Procedures of Swahili Terminology Development in Tanzania: A re- Examination of Basic Issues". *Journals of Asian and African Studies* 38: Uk. 161-176.

- Mwansoko, H.J.M. (2007) “Ukweli kuhusu Hali ya Tatizo la Istilahi za Kufundishia Elimu ya Sekondari na Juu”. Katika Tumbo- Masabo na Chiduo (Wah.) *Kiswahili katika Elimu*. Dar es Salaam; TUKI: Uk.144-154.
- Sewangi, S. S. (2007) “Uundaji wa Istilahi za Kiswahili Kileksikografia na Athari zake” *Nordic Journal of African Studies* 16 (3), Uk. 333-344.
- TUKI (2013) *Kamusi ya Kiswahili Sanifu (Toleo la Tatu)*. Nairobi: Oxford University Press.
- TUKI (2016) *Majina ya Vitengo na Nyadbfifa za Viongozi*. Dar es Salaam: TATAKI.
- Tumbo-Masabo, Z. N na Mwansoko, H. J. (1992) *Kiongozi cha Uundaji wa Istilahi za Kiswahili*. Dar es Salaam: TUKI.
- UNESCO (2005) *Guideline for Terminology Policies: Formulating and Implementing Policy Language in Communities*. UNESCO/Infotem. Paris.
- Were-Mwaro, A.G. (2000) Usayansi wa Istilahi za Isimu ya Kiswahili: Tasnifu ya Uzamivu (*Haijchapishwa*). Chuo Kikuu cha Egerton. Nairobi.
- Were-Mwaro, A.G. (2002) “Tathmini ya Nadharia za Uundaji wa Istilahi za Kiswahili”. *MULIKA* 26, Dar es Salaam: TUKI. Uk. 62-74.

